# LONDA

## NIGERIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE



## RIPOTI YA 2020

www.paradigmhq.org

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

# LONDA

## NIGERIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

**Imechapishwa na Paradigm Initiative**
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org

Iliyochapishwa mnamo Aprili 2021

Ripoti iliyotolewa na Adeboye Adegoke na Judith Takon
Timu ya Uhariri: 'Gbenga Sesan, Kathleen Ndongmo, Koliwe Majama, Margaret Nyambura Ndung'u, Mawaki Chango, Nnenna Paul-Ugochukwu and Thobekile Matimbe.
Ubunifu na Luce Concepts

This publication may be reproduced for non-commercial use in any form provided due credit is given to the publishers, and the work is presented without any distortion.

Copyright © 2021 Paradigm Initiative

Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)



# LONDA

**NIGERIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

## YALIYOMO


UTANGULIZI 1

MKAKATI WA SERA YA UCHUMI WA KIDIJITALI 2

ATHARI YA KANUNI ZA COVID-19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI 3

FARAGHA, KITAMBULISHO CHA KIDIJITALI NA UFUATILIAJI 4

UHURU WA KUJIELEZA MTANDAONI NDANI YA 2020 6

KIWANGO CHA KUTENGWA NA ATHARI ZAKE KWA HAKI ZA BINADAMU 8

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 9

UTAFITI MAALUM 10


Asasi za kiraia zinaendelea kufanya kazi ili kuendeleza haki za dijitali na ujumuishi barani Afrika, kuhakikisha njia bora zinapitishwa katika sera na sheria. Ripoti hii inachambua hali ya haki za dijitali na ujumuishi nchini Nigeria, ikichunguza ukiukaji na mapungufu, ikiangazia utumiaji na utekelezwaji wa sera na sheria, ikiangazia hatua muhimu na kutoa mapendekezo kwa mandhari ya dijitali nchini Nigeria. Pamoja na ripoti kutoka nchi 20, toleo hili linaangazia kati ya maswala mengine, pengo la kidijitali lililozidishwa na janga la COVID-19 na kufichua ukiukaji kwenye nyanja tofauti kama vile faragha, ufikiaji wa habari, na uhuru wa kujieleza na msingi wa sheria na sera ulioelezewa vizuri.

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ



Nigeria inatajwa kama nchi yenye uchumi mkubwa sana barani Afrika,[1] yenye Kipato cha Taifa cha wastani cha Naira milioni 39,089,460.61, sawa na Dola za Marekani ($100,611.0703)[2] kwa viwango vya kawaida.[3] Na idadi ya watu milioni 208,[4] Nigeria ina maliasili kadha ikiwa ni pamoja na mafuta yasiyosafishwa, gesi asilia, makaa ya mawe, chuma na bati.

UTANGULIZI

# HAKI ZA DIJITALI NA UJUMUISHAI YA NCHI YA NIGERIA

Kwa miaka mingi, uchumi wa nchi umekuwa ukitegemea sana mapato kutoka kwa mafuta yasiyosafishwa, hata hivyo, kushuka kwa bei ya mafuta ulimwenguni katika nyakati za hivi karibuni na athari yake, iliyochangiwa na ongezeko la umasikini na uasi, nchi imejikita katika kupanua uchumi kwa kuanza kuelekeza darubini kwenye sekta yake zisizo za mafuta, haswa kilimo, huduma za kifedha na mawasiliano ya simu / TEHAMA. Kushuka kwa bei ya mafuta yasiyosafishwa na upungufu wa uzalishaji wa mafuta kwa kiasi kikubwa kumechangia kushuka kwa uchumi kwa nchi mnamo 2016,[5] kwa mara ya kwanza tangu 1991.

**14.3%**
**ilichangiwa na tasnia ya mawasiliano kwa Pato la Taifa la Nigeria kama Q2 2020**

Athari za COVID-19 kwa uchumi wa Nigeria zimekuwa kubwa na ingawa tasnia nyingi ziliandikisha hasara kubwa, tasnia ya TEHAMA / Mawasiliano ni moja wapo wa ile iliyoepuka athari za janga hilo, kwani ilishuhudia ukuaji wa haraka kwa sababu ya ongezeko la uhitaji.[6] Takwimu za Tume ya Mawasiliano ya Nigeria (NCC) zinaonyesha kuwa tasnia ya mawasiliano ilichangia 14.3% kwa Pato la Taifa la

1. https://www.bloomberg.com/news/articles/2020-03-03/nigeria-now-tops-south-africa-as-the-continent-s-biggest-economy.
2. Official exchange rate as at the 18th of December 2020 - 1 USD = 388.520
3. National Bureau of Statistics. "Nigerian Gross Domestic Report (Q3 2020)" .
4. https://www.worldometers.info/world-population/nigeria-population/
5. According to the Nigerian National Bureau of Statistics GDP Q4 2016 Report, there was a steady decline in the economy from Q1 2015 to Q4 2016.
6. According to statistics from the Nigerian Communication Commission, active internet subscriptions increased from 128,723,188 in January 2020 to 136,114,413 in March 2020 to 147,148,307 by July 2020 when some states in the country began easing restriction measures, shorturl.at/elCGP [Accessed 7 January 2020]

Nigeria hadi kufikia kipindi cha robo ya 2 cha mwaka wa 2020, kutoka 10.6% kwenye robo ya 4 ya 2019. Ukuaji huu umekuwa hivi, kwani tasnia imeshuhudia ongezeko la uhitaji la huduma za mtandao na mawasiliano. Hii inaelekezea utegemeaji wa nyezo hizi mawasiliano kupunguza, kwa kiwango fulani, athari ya COVID-19, haswa kwa kuwa inahusiana na mazingira ya biashara na mwingiliano wa kijamii. Mbali na umuhimu wazo kwa wafanyabiashara na mwingiliano wa jumla wa kijamii katika kipindi hiki, teknolojia za kidijitali kwa ujumla zimesaidia sana katika urushaji habari, burudani, huduma za kifedha, utetezi, na shughuli zinginezo nchini Nigeria.

Utegemeaji nyenzo hizi za kidijitali umeonyesha umuhimu wazo kwa Nigeria. Pamoja na orodha inayoongezeka ya mwingiliano katika nyanja ya kidijitali, umuhimu wa utawala bora wa sheria unahitaji kutiliwa mkazo zaidi. Uwepo wa Wanigeria katika ulimwengu wa kidijitali kunamaanisha kuhatarishwa na aina mpya ya vitisho kwa haki zao, ambavyo vinaweza kufanya sheria zilizopo kukosa kujitosheleza. Ili kulinda maslahi ya Wanigeria mtandaoni, Bunge za utungaji sheria sheria na idara husika za serikali zimekuwa zikifanya juhudi kuunda mazingira mwafaka ya kisheria. Pamoja na mazungumzo juu ya ulindaji haki za Wanigeria mtandaoni, linajitokeza swala la umuhimu wa ujumuishaji. Na faida zote zinazotambulika za uchumi wa kidijitali, vizuizi vya ufikiaji vinamaanisha kutengwa na faida hizi. Kwa nchi inayoendelea kama Nigeria, iliyo na karibu 40% ya idadi ya watu wanaoishi chini ya kiwango cha umaskini, majadiliano yanayohusu ujumuishaji wa kidijitali yanapaswa kuwa mada muhimu. Yote haya yanayafanya mazungumzo yanayohusu haki za kidijitali na ujumuishaji kuwa zenye muhimu kwa demokrasia na udhabiti wa uchumi wa Nigeria.



## MKAKATI WA SERA YA UCHUMI WA KIDIJITALI

Mnamo Oktoba 2019, serikali ya Nigeria ilibadilisha jina la Wizara yake ya Mawasiliano kuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchumi wa Kidijitali katika hatua ambayo iliashiria kuwa nchi imetambua umuhimu wa uchumi wa kidijitali kwa ustawi wa uchumi wake. Mnamo Juni 2020, nchi hiyo ilitoa sera na mkakati wa kitaifa wa uchumi wa kidijitali "kugeuza Nigeria kuwa uchumi unaoongoza wa kidijitali unaotoa maisha bora na uchumi wa kidijitali kwa wote". Hata hivyo, katika kile kinachoonekana kama mgogoro, Nigeria imechukua hatua, katika kipindi hichi, kudhibiti nyanja za kidijitali. Nchi imekuwa ikishinikiza udhibiti wa mitandao ya kijamii. Wakati wa ripoti hii ikiandikwa, kuna kanuni mbili zilizopendekezwa zinazolenga kudhibiti "matamshi ya chuki"[7] na kupambana na "habari bandia"[8] nchini Nigeria. Miswada hii miwili, kama inavyozingatiwa na Kamati ya Kulinda Wanahabari, inalenga kuzuia uhuru wa raia nchini Nigeria. Kwa mfano, Muswada wa Ulindaji dhidi ya Uongo na Udanganyifu wa Mtandaoni, unaipa serikali, kupitia Jeshi la Polisi la Nigeria, nguvu ya kuzuia ufikiaji huduma za mtandao na kubaini uongo huo au habari zingine zinazoshirikiwa na raia wa Nigeria kwenye majukwaa ya kidijitali.

7. The Hate Speech (Prohibition) Bill 2019 has passed the first reading https://www.nassnig.org/documents/bill/10613.
8. The Protection from internet falsehoods and manipulation and other related matters Bill 2019 has passed the second reading, https://placbillstrack.org/view.php?getid=6649

Kujumuishwa kidijitali kumekuwa ni suala la haki za kidijitali. Msimamo huu umeimarishwa zaidi na hali halisi ya janga la COVID-19 na mapungufu yanayotokana na janga hili. Uwezo wa kujifunza, kushiriki, kufanya kazi na kufanya biashara ulitegemea uunganishwaji mtandaoni na uwezo wa kutumia vifaa na majukwaa ya kidijitali. Wale ambao hawakuweza kumudu ufikiaji mtandao au ambao hawangeweza kutumia vifaa vya kidijitali huenda shughuli za maisha yao zilisitishwa. Mwanzoni mwa utekelezaji wa hatua za kufungwa, viongozi wa vitengo vya shirikisho vya Nigeria, Jukwaa la Magavana la Nigeria, walianza kutekeleza makubaliano ya mapema na wadau wa mawasiliano ili kupunguza gharama ya ya haki ya njia, yaani Right of Way (RoW).[9] Gharama ya RoW kwa muda mrefu imekuwa ikitambuliwa kama moja ya vizuizi vya kuhakikisha uunganishaji wa mtandao wa kutegemewa katika maeneo ya vijini nchini Nigeria.[10] Kulingana na Tume ya Mawasiliano ya Nigeria (NCC), Nigeria inahitaji takriban kilomita 120,000 za nyaya za mkonga kufikia lengo lake la ufikiaji mtandao lakini ni takriban kilomita 38,000 tu za nyaya zilizowekwa.[11] Uunganishaji mtandao lilikuwa hitaji muhimu la miundombinu kuhakikisha wanafunzi wanaendelea na masomo kwani shule zilifungwa kama sehemu ya hatua za kufunga nchi, na athari kwa haki ya wanafunzi kupata elimu.

“Kujumuishwa kidijitali kumekuwa ni suala la haki za kidijitali.”

Umuhimu wa ujumuishaji kidijitali ni wa kusisitizwa mno. Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) 2020-2030[12] ni pamoja na ujumuishaji kidijitali[13] kama sehemu ya mpango kuelekea ustawi wa ulimwengu, haswa kuendeleza ujumuishaji katika nchi zenye maendeleo duni. Ripoti iliyochapishwa na Ofisi ya Takwimu ya Nigeria mnamo Mei 2020 inaonyesha kwamba 40% ya idadi ya watu, au karibu watu milioni 83, wanaishi chini ya kiwango cha umaskini wa nchi hiyo wa naira 137,430 ($ 381.75) kwa mwaka.[14]

> Kwa hivyo, ujumuishaji ni muhimu ili kufanikisha uwezo wa kiuchumi wa Nigeria. Wanigeria waliotengwa kidigitali wanaweza kukosa ujuzi, ujasiri na motisha, pamoja na kuwa na ufikiaji mdogo au kutofikia kabisa vifaa na uunganishaji. Hii inaunda matabaka ya ziada ya jamii zinazotengwa na huzidisha matatizo ya kijamii na kiuchumi.

## ATHARI YA KANUNI ZA COVID-19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI

Ili kudhibiti kuenea na kupunguza athari ya virusi vya COVID-19, serikali ya shirikisho ya Nigeria ilitekeleza hatua kadha za kiafya, kijamii, na kiuchumi ikiwemo pamoja na marufuku ya kusafiri, vizuizi vya uhamaji na utoaji wa chakula na msaada wa kifedha, kati ya vinginevyo. Kwa kawaida, kutangazwa kwa hatua zilizolenga kuzuia kuenea kwa virusi vya corona kulionekana kana kwamba kumezalisha uga wa kukiuka haki za kidijitali pamoja na haki za faragha na uhuru wa ufuatiliaji haramu. Kuongezeka kwa viwango vya ufuatiliaji, kuzuia uhuru wa kusema na usimamizi mbaya wa

9. https://nairametrics.com/2020/01/25/state-governors-finally-agree-to-reduce-row-charges-for-telcos/
10. https://www.nigeriacommunicationsweek.com.ng/right-of-way-issues-frustrate-broadband-penetration/
11. https://www.thecable.ng/ncc-need-120000km-optic-fiber-network-38000km-covered
12. The 2030 Agenda for Sustainable Development seeks to build on the Millennium Development Goals, a United Nations agenda geared to meet the needs of the world's poorest by the year 2015. The 2020 agenda sets out to achieve sustainable development in its three dimensions – economic, social and environmental – in a balanced and integrated manner by the year 2030.
13. Target 9.c: Access to ICT - Significantly increase access to information and communications technology and strive to provide universal and affordable access to the Internet in least developed countries by 2020.
14. http://nigerianstat.gov.ng/download/1092




> *"Umuhimu wa ujumuishaji kidijitali ni wa kusisitizwa mno. Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) 2020-2030 ni pamoja na ujumuishaji kidijitali kama sehemu ya mpango kuelekea ustawi wa ulimwengu, haswa kuendeleza ujumuishaji katika nchi zenye maendeleo duni.*

taarifa / data ya kibinafsi ni baadhi ya ukiukaji ambao Wanigeria wamekuwa wakishughulikia katika kipindi hiki.[15] Kwa mfano, Waziri wa Mawasiliano na Uchumi wa Kidijitali aliripotiwa kutaja uchimbaji wa data, kulingana na data ya usajili wa kadi za SIM, kama njia ya kutambua hali ya kifedha ya Wanigeria ili kutoa msaada ufaao. Katika tukio jingine la ukiukaji wa wazi wa faragha, Waziri wa Masuala ya Kibinadamu na Usimamizi wa Maafa, Sadiya Farouq, katika mkutano na waandishi wa habari Ikulu, alifichua mipango ya kutoa msaada wa kifedha kwa Wanigeria wakitumia habari inayopatikana moja kwa moja kutoka kwa Nambari ya Uthibitishaji ya Biometri (BVN) iliyounganishwa na akaunti za benki na data ya siri iliyotolewa kwa mitandao ya rununu.

## FARAGHA, KITAMBULISHO CHA KIDIJITALI NA UFUATILIAJI

Ibara ya 37 ya Katiba ya Nigeria ya 1999 inahakikishia faragha ya raia, nyumba zao, mawasiliano, mazungumzo ya simu na mawasiliano ya telegrafu.[16] Haki ya faragha nchini Nigeria inahimiliwa na Azimio la Ulimwenguni la Haki za Binadamu (UDHR) na Kifungu cha 17 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR). Ingawa kifungu katika katiba hakijataja "data" haswa,taarifa kuhusu nyumba zao, mawasiliano na mazungumzo ya simu yamenakiliwa katika ufafanuzi wa data ya kibinafsi.[17]

Tume ya Kitaifa ya Usimamizi wa Vitambulisho

15. https://www.icirnigeria.org/covid-19-controversy-trails-ministers-decision-to-mine-data-of-phone-users-without-consent/
16. Lfn
17. Olumide Babalola, Data Protection And Privacy Challenges In Nigeria (Legal Issues). March 9, 2020, available at https://www.mondaq.com/nigeria/data-protection/901494/data-and-privacy-challenges-in-nigeria-legal-issues-

(NIMC) ilitangaza mipango ya kuunda mfumo wa kidijitali ili kuunda mazingira wezeshi ya uandikishaji mzuri wenye mafanikio wa raia wa Nigeria na wakaazi halali nchini Nigeria. Mfumo huo utakuwa hifadhidata salama ya kitambulisho cha kitaifa ambapo vitambulisho vya kidijitali vitapewa kila mtu kwa njia ya Nambari ya Kitambulisho cha Kitaifa (NIN).[18] Utaratibu huu umeendelea licha ya ukosefu wa kutosha wa kisheria wa ulindaji data za kibinafsi. Ingawa Sheria ya Ulindaji Data ya Nigeria (NDPR) ilitolewa na Idara ya Kitaifa ya Habari Teknolojia Maendeleo mnamo 2019, haionyeshi mchakato kamili wa utunzaji wa data kwani haigusii uanzishwaji wa wa tume huru ya ulindaji data.

Ingawa Kanuni za Kimataifa kuhusu Utekelezaji wa Haki za Binadamu kwenye Ufuatiliaji[19] wa Mawasiliano inataja wakati mipaka inatumika kwa haki ya faragha, shirika la sheria nchini Nigeria[20] lina vifungu kadhaa juu ya haki ya kisheria ya serikali ya ufuatiliaji, na serikali ya Nigeria ina historia ya ufuatiliaji wa ziada kwa raia wake.

> **"Kwa hivyo, ujumuishaji ni muhimu ili kufanikisha uwezo wa kiuchumi wa Nigeria."**



Ripoti ya uchunguzi ya Citizen Lab, maabara ya taaluma mbali mbali iliyoko katika Munk School of Global Affairs and Public Policy katika Chuo Kikuu cha Toronto nchini Canada iliripoti kuwa Nigeria imepata Signaling System 7 (SS7), Safu ya itifaki iliyoundwa kwa ajili ya kubadilishana habari na kupeleka mawasiliano ya simu kati ya kampuni tofauti za mawasiliano ya simu.[21]

Kwa bahati mbaya, hii sio tukio la mara moja nchini Nigeria[22] Ufuatiliaji wa ziada wa kimahakama unaoongozwa na serikali ni ukiukaji wa jukumu la serikali kuhifadhi haki ya ndani ya faragha, na ulinzi kutoka kwa kuingiliwa holela kwa faragha ya raia wake.

18. NIMC website, https://www3.nimc.gov.ng/digital-identity-ecosystem/
19. Section 45 of the 1999 Constitution, the Terrorism (Prevention) Act (Ammended 2013) and the CyberCrime (Prevention) Act, 2015
20. Full investigative report available at
https://citizenlab.ca/2020/12/running-in-circles-uncovering-the-clients-of-cyberespionage-firm-circles/
21. DSS Bugs 70% Of Mobile Phones In Abuja, https://www.independent.ng/dss-bugs-70-mobile-phones-abuja/
22. DSS Bugs 70% Of Mobile Phones In Abuja

## UHURU WA KUJIELEZA MTANDAONI NDANI YA 2020

Haki ya uhuru wa kujieleza, pamoja na uhuru wa kushikilia maoni na kupokea na kutoa maoni na habari bila kuingiliwa inaungwa mkono kikatiba na Ibara ya 39 ya Katiba ya Nigeria ya 1999.[23] Kifungu hicho kinazidi kuelezea zaidi kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki, kuanzisha na kutumia njia yoyote kwa usambazaji wa habari,mawazo na maoni.[24] Kwa kuzingatia hili, ukiukaji unaoungwa mkono na serikali wa haki ya kujieleza mtandaoni ni kinyume na mamlaka yake ya kulinda haki hii. Mfano madhubuti wa ukiukaji huu ni kuwekewa vikwazo na Tume ya Kitaifa ya Utangazaji kwenye vituo vitatu vya runinga vya Nigeria, Channel TV, Arise TV na Televisheni Huru ya Afrika (Africa Independent Television) kwa kurusha video zilizopatikana kutoka kwa "vyanzo vya habari vya kijamii visivyo na uthibitisho".[25]




Kumekuwepo na ripoti kadha za kukamatwa kunatokana na utumiaji wa majukwaa ya mitandao ya kijamii. Babatunde Olusola, mwanafunzi wa chuo kikuu, alikamatwa kwa madai ya kuendesha akaunti ya kuiga, kwa jina la Rais wa zamani wa Nigeria, Goodluck Jonathan, kwenye Twitter.[26] Sheria za Twitter zinasema kuwa watumiaji wanaruhusiwa kuunda akaunti ya kuiga, huduma ya habari zinazotolewa mara kwa mara, maoni, na akaunti za mashabiki kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii, mradi akaunti hizo zinafuata vigezo fulani, ikiwemo pamoja na kusema kuwa akaunti hiyo haihusiani na mlengwa wa akaunti ya kuiga.[27] Babatunde Olusola alifuata vigezo hivi kwa kuweka 'SIO GEJ'[28] kwenye wasifu wa akaunti hiyo ya kuiga ya Twitter, kama tangazo la kutoshirikiana na Rais huyo wa zamani lakini bado alikamatwa[29] Kulikuwa pia na matukio mengine mengi ya kukamatwa kwa raia wa Nigeria kwa kuandamana dhidi ya ukatili wa polisi kama sehemu ya maandamano yaliyoongozwa na vijana yaliyofanyika mnamo Oktoba 2020, yenye kibwagizo cha #EndSARS.




Na uungwaji mkono na haki ya kujieleza mtandaoni, Wanigeria

23. 1999 constitution
24. Section 39(2) of the Constitution. The exemption to this right is the right to own, establish or operate a television or wireless broadcasting station for any purpose whatsoever.
25. https://www.premiumtimesng.com/news/more-news/423162-endsars-nbc-imposes-n3m-sanction-each-o n-ait-channels-arise-tv.html
26. Story available at punch newspaper online https://punchng.com/student-arrested-for-opening-jonathan-parody-account-denied-access-to-lawyers/ accessed
27. Twitter rules on Parody accounts, https://help.twitter.com/en/rules-and-policies/parody-account-policy
28. The initials of Former President Goodluck Ebele Jonathan
29. There were multiple reports of indiscriminate arrests of Nigerian citizens protesting against the Special Anti-Robbery Squad. Report available at https://cutt.ly/SjkXezw [Last accessed 8 January 2021]

wanatumia mitandao ya kijamii na majukwaa ya mtandaoni kuzungumza kuhusu maswala muhimu nchini. Harakati ya #EndSARS iliyotajwa hapo awali ambayo ilianza tena mnamo 2020 baada ya video ambayo haijathibitishwa ya afisa wa polisi wa SARS akimpiga risasi kijana Mnigeria ilivuma mtandaoni, ilipokea msaada mkubwa, wa kifedha na vinginevyo kutoka kwa Wanigeria, Wanigeria walioko ughaibuni na jamii ya kimataifa. Harakati zinazoungwa mkono kidijitali kama hii sio jambo jipya nchini Nigeria. Mnamo mwaka wa 2012, pamoja na maandamano ya mitaani, Wanigeria walitumia mitandao ya kijamii kuelezea kutoridhishwa kwao na kuondolewa kwa ruzuku ya mafuta kwa kutumia kibwagizo cha #OccupyNigeria.[30]

Kibwagizo cha #BringBackOurGirls[31] kiliangazia kampeni ya kuwarudisha wasichana wa shule 276 waliotekwa nyara kutoka Chibok, kijiji katika Jimbo la Borno, Nigeria, na kundi la wanamgambo wanaojulikana kama Boko Haram mnamo 14 Aprili, 2014. Kampeni ya mtandaoni ya #NoTooYoungToRun ilitumiwa na Wanigeria kutetea ujumuishaji pakubwa wa vijana katika Bunge nchini Nigeria, kampeni ambayo ilisababisha kupitishwa kwa Sheria ya Kupunguza Umri, maarufu kama Sheria ya Si Mdogo Sana Kugombea. Matumizi ya mitandao ya kijamii kama nyenzo ya uanaharakati kuangazia maswala haya na mengine nchini Nigeria si ya kupuuziwa.

Katika jaribio la kudhibiti mazingira ya mtandaoni nchini Nigeria, Bunge za utungaji sheria zinajaribu kupitisha Ulindaji kutokana na Uongo wa Mtandao,Ushawishi na Muswada wa Makosa mengine,[32] uliopewa jina la utani Muswada wa Mtandao wa Jamii.[33] Vipengele vya muswada huo vinalenga kuhalalisha urushaji wa 'taarifa za uwongo' kama ilivyoainishwa katika muswada huo kwa nia ya kuzuia kuenea kwa habari potofu na habari bandia. Wakosoaji wa muswada huo wameelezea kuwa vifungu vilivyomo ni jaribio la kukandamiza uhuru wa kujieleza mtandaoni na kunyamazisha wenye maoni tofauti na serikali.[34] Kinyume chake, Muswada wa Haki za Kiditali na Uhuru wa 2019, kama sehemu ya malengo yake, ulindaji wa uhuru wa kujieleza, kukusanyika na kutangamana mtandaoni.

Muswada huo ulipitishwa na Bunge zote mbili mnamo 2019, hata hivyo, Rais alikataa kutia saini muswada huo kwa madai kwamba "unajumuisha masuala mengi yanayoshindwa kushughulikia lolote kati kiundani zaidi."[35] Muswada huo umerekebishwa sasa, lakini utalazimika kupitia michakato ya kutunga sheria tena kabla ya kupata nafasi ya kutiliwa saini kuwa sheria. Kutia saini muswada huu kuwa sheria itakuwa hatua mwafaka katika kulinda uhuru wa kujieleza mtandaoni, na kuwapa raia mchakato kamili wa kisheria wa kutafuta haki iwapo kuna ukiukwaji.

> **"Kinyume chake, Muswada wa Haki za Kiditali na Uhuru wa 2019, kama sehemu ya malengo yake, ulindaji wa uhuru wa kujieleza, kukusanyika na kutangamana mtandaoni."**

30. Occupy Nigeria Protest, available at https://cutt.ly/2jzrI76 [Last accessed 9th January 2021]
31. Chibok Schoolgirls Kidnapping, available at https://cutt.ly/pjzeISO [Last Accessed 9th January 2021]
32. Protection from Internet Falsehood, Manipulations and Other Offences Bill
33. The bill has passed second reading in the Senate but the report of a March 2020 Public Hearing has not been released.
34. There is currently a petition to kill the bill https://www.change.org/p/the-national-assembly-of-the-federal-republic-of-nigeria-stop-the-social-media-b ill-you-can-no-longer-take-our-rights-from-us
35. President Buhari in his letters to the Senate on his decision to decline the Digital Rights and Freedom bill mentioned that the bill covers too many technical subjects and "fails to address any of them extensively. News available at https://cutt.ly/NjkThwv [Last accessed 8 January 2021]

## KIWANGO CHA KUTENGWA NA ATHARI ZAKE KWA HAKI ZA BINADAMU

Dhana ya ujumuishaji wa kijamii inajumuisha ufikiaji sawa wa nyenzo na rasilimali na wanajamii. Kwa upande mwingine, kutengwa kwa jamii kunatoa wazo la kutengwa kwa wanajamii kutoka kwa ufikiaji wa nyenzo hizi. Katika karne ya 21, nyenzo za kidijitali zimekuwa sehemu muhimu ya maisha ya wanadamu, kuanzia utandawazi wa uchumi hadi kuleta mapinduzi ya mwingiliano wa kijamii.

Kama ilivyotajwa hapo awali, tasnia ya mawasiliano peke yake ilichangia hadi 14.3% kwa Pato la Taifa la Nigeria katika nusu ya kwanza ya 2020. Hakika, pamoja na manufaa yote za mageuzi ya kidijitali, kutengwa na ufikiaji kunakinzana na nadharia muhimu ya ujumuishaji wa kijamii. Manufaa yote mazuri ya mtandao hujidhihirisha yenyewe baada ya teknolojia kufikiwa na idadi ya watu imejifunza jinsi ya kutumia teknolojia angalau kwa kiwango cha msingi sana.[36] Kuangazia umuhimu wa ujumuishaji kidijitali, Lengo la Maendeleo Endelevu 9 inatambua kuongeza ujumuishaji wa kidijitali katika nchi zinazoendelea[37] kama lengo. Nigeria inachukuliwa kama nchi inayoendelea, na yenye 40% ya idadi yote ya watu wanaoishi chini ya kiwango cha umaskini.[38]



> *Katika karne ya 21, nyenzo za kidijitali zimekuwa sehemu muhimu ya maisha ya wanadamu, kuanzia utandawazi wa uchumi hadi kuleta mapinduzi ya mwingiliano wa kijamii.*
> ”

Mbali na ufikiaji wa faida za kiuchumi kama inavyotolewa na upatikanaji na utumiaji wa nyenzo za kidijitali, kutengwa kidijitali kunakatisha vikundi kadhaa vya watu kufurahia haki za kimsingi za kibinadamu kama vile haki ya kushiriki katika serikali na uchaguzi huru, haki ya kupata elimu, haki ya viwango tosha vya maisha, na haki ya usalama wa kijamii katika muktadha wa sasa. Kwa mfano, mfumo unaopendekezwa ya kidijitali nchini Nigeria unamaanisha kwamba wasiojua kusoma / waliotengwa wanaweza kukosa nyenzo za kupigia kura, kufungua akaunti za benki au kupokea habari fulani. Sababu kadhaa zinasababisha kutengwa kidijitali, pamoja na ulemavu, viwango vya kusoma na kuandika, umaskini, utamaduni na lugha. Watu waliotengwa kwa njia ya kidigitali wanaweza kukosa ujuzi, ujasiri na motisha, pamoja na kuwa na ufikiaji mdogo au kutokuwa na ufikiaji kwa nyenzo na uunganishwaji. Hii inaweza kuunda matabaka ya ziada ya kutengwa kwa jamii na kuzidisha matatizo ya kijamii na kiuchumi.[39]

36. The Digital Divide and Human Rights - What the EU should do at the World Summit on Information Society, (2005) Anne Peacock, a doctoral researcher in the Law Department of University of Essex, available at https://cutt.ly/9hTDNfi
37. Sustainable development Goal 9c - Significantly increase access to information and communications technology and strive to provide universal and affordable access to the Internet in least developed countries by 2020, https://sdgs.un.org/goals/goal9
38. Statistics from the National Bureau of Statistics, available at 2019 POVERTY AND INEQUALITY IN NIGERIA.cdr - National ...nigerianstat.gov.ng › download [Accessed 9 December 2020]
39. Missing footnotes

Upenyo wa mtandao nchini Nigeria ulikuwa 42% kufikia Januari 2020. Mkakati wa Sera ya Kitaifa ya Uchumi wa Kidijitali 2020-2030[40] unalenga 70% ya upenyaji wa broadband[41] katika miaka 4.[42] Baadhi ya mikakati ya kufanikisha lengo hili ni pamoja na kukuza kanuni nzuri za TEHAMA na sekta ya kidijitali kwa njia inayowezesha maendeleo, kuboresha ufahamu wa kidijitali, kuweka miundombinu ya kudumu na ya rununu ili kuimarisha upenyaji wa broadband nchini na kuhimili huduma za kidijitali za serikali. Kufanikiwa kwa mkakati huu kutaleta faida kama vile ujumuishaji mkubwa wa kidijitali.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Katika karne ya 21, nyenzo za kidijitali zimekuwa sehemu muhimu ya maisha ya wanadamu, kuanzia utandawazi wa kibiashara hadi kuleta mageuzi ya mwingiliano wa kijamii. Kama ilivyotajwa hapo awali, tasnia ya mawasiliano / TEHAMA peke yake ilichangia hadi 14% kwa Pato la Taifa la Nigeria. Sekta kuafikia kiwango hiki cha ushawishi na upenyaji wa 42% tu ni kiashiria tosha cha manufaa yake ya kiuchumi kwa uchumi wa Nigeria. Kama ilivyochapishwa hapo awali, pamoja na faida zote za mageuzi ya kidijitali, kutengwa na ufikiaji kunakinzana na nadharia muhimu ya ujumuishaji wa kijamii. Pia, inakubalika kuwa TEHAMA hutoa michango anuwai ya kimsingi na ya kimfumo inayowezesha maendeleo endelevu na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).[43] Na uhusiano uliobainishwa kati ya uchumi, ujumuishaji wa kijamii na nyenzo za TEHAMA / kidijitali, juhudi za ujumuishaji wa kidijitali, ulindaji wa haki mtandaoni na uwekezaji katika tasnia ya TEHAMA/ mawasiliano na serikali ya Nigeria na wadau katika tasnia hiyo ni muhimu sana.

Ukuzaji matumizi ya TEHAMA / nyenzo za mawasiliano hakutakuwa kamili bila ya kusisitiza tena jukumu la taifa la kuhifadhi haki za raia wake kwenye majukwaa haya. Hoja ya kutunga sheria na sheria tanzu ambayo inalinda vya kutosha waliounganishwa kidijitali na kukuza ujumuishaji wa kidijitali hakuwezi kupuuziwa kabisa. Kuna pia hali ya jumla ya kutokuamini vyombo vya kutekeleza sheria na mfumo wa kimahakama nchini Nigeria na umma, haswa wale wasio na uwezo. Pamoja na kutokuamini kiwango cha kutokujua kusoma na kuandika ambacho huathiri uelewa wa haki bila kukusudia, huzuia uwezo wa kudai haki hizi.[44] Katika kukuza au kuongeza imani katika michakato ya kimahakama, Nigeria ingefaidi na kampeni za uhamasishaji kuhusu haki za binadamu, nje ya mtandao na mtandaoni, iliyoelekezwa haswa kwa wale ambao wanaweza kuwa wamepewa taarifa potofu kuhusu haki zao, au wale ambao hawana ufahamu kuzihusu, na kuhakikisha ufikiaji wa haki wakati ukiukaji unatokea.

40. About digital inclusion and exclusion, Citizens Online Webpage, https://www.citizensonline.org.uk/digital-inclusion/ [Accessed 9 December 2020]
41. The National Digital Economy Policy Strategy 2020-2030, developed by the Nigerian Communications Commision,
42. 2020 – 2024 Nigeria's National Digital Economy Policy and Strategy
43. How ICT Can Accelerate the Implementation of the Sustainable Development Goals by Darine Ameyed, November 8, 2018. Available at https://cutt.ly/ojczSZW . ]Last Accessed 10 January 2021]
44. There is a link between literacy and the assertion of human rights in Nigeria as posited by Apeh, Elaigwu Isaac (Ph.D) in his paper 'Literacy Promotion for Human Rights Awareness and Protection - The case for Nigeria', available at https://cutt.ly/fjcs8AS [Last accessed 9th January 2020]

## Utafiti Maalum: Tishio kwa faragha ya data kwa Wanigeria kwenye janga

Imeandaliwa na Khadijah El-Usman

Nigeria ilirekodi kisa chake cha kwanza cha COVID-19 mnamo February 2020 na kama nchi zingine, ikalazimika kukusanya rasilimali kuweza kupambana na madhara yaliyotarajiwa kutokea. Na kwa madhara yasiyokusudiwa kulijitokeza hatua zisizokusudiwa. Serikali zililazimika kutambua kwa haraka na kuhakikisha huduma kwa visa, kufuatilia na kuwafanyia karantini wawasiliani wao na kufuatilia mienendo ya janga. Nchi kama Ubeljiji, Malaysia, na Singapore ziliunda programu za mtandaoni na kutumia vifaa vya simu kufuatilia wananchi wao.

Nigeria, kwa upande mwimgine, imekuwa na historia ya kutatanisha ya ufuatiliaji wa afya bila kuzingatia haki kwa faragha binafasi. Hili lilijidhihirisha kwenye kongamano la magavana lililojaribu kutumia kampuni za simu kama vile MTN kufuatilia harakati za watu, hadi programu kama vile Stay-SafeNG zikiundwa kwa minajili ya ufuatiliaji wa COVID-19.

Kwa Mnigeria wa kawaida aliyeathirika na COVID-19, kushudia kwao kwa ufuatiliaji wa afya kulikuwa kwa kiwango kidogo ila kulisaidia kutoa upeo mkubwa wa tatizo lililopo. Kwa Dr Ade (jina limebadilishwa), baada ya yeye na wenzake wachache walipokumbwa na dalili sawa na za COVID-19 na kupatikana na virusi baada ya kupima, hospitali ilitekeleza ufuatiliaji wa wasiliani kwake na kwa wenzake. Aliielezea hatua kama "kufanya michoro ya venn (venn diagarams) yenye nguzo kwa wagonjwa wote tuliokutana nao" na hatimaye kugundua kuwa madaktari wote kwenye kitendawili walikuwa wamekutana na mgonjwa yule yule.

Hospitali ilikuwa na kitengo chake cha COVID-19 kilichoripoti katika kituo cha taifa cha Nigeria Centre for Disease Control (NCDC) ambacho kilifanya ufuatiliaji wa wawasiliani. Ade alisema, "Hospital yangu ina uwezo maalum wa kuzifanya taarifa zote za wagonjwa kuwa dijitali kwa hivyo ilikuwa rahisi kupata taarifa za mawasiliano za wagonjwa waliohusika," kumaanisha mashirika tofauti na kitengo cha COVID-19 yaliweza kufikia taarifa za wahusika bila idhini yao. Alielezea zaidi kwamba kutokana na ufahamu wake wa masuala ya magonjwa ya kuambukizwa, "unapopambana na ugonjwa wenye hali ya juu ya kuambukiza, unaweza kupata maelezo ya mgonjwa yanayohusiana na swala

hilo, kumaanisha anwani na nambari ya simu." Na hilo akilini, ni la kustaajabisha mbona jimbo la Lagos State, Chuo cha Nigeria cha Utafiti wa Afya (Nigerian Institute of Medical Research) kiliunda fomu ya Google yenye kurasa saba iliyohitajika kujazwa na wale wote waliohitaji vipimo vya COVID-19 wakati janga lilipokuwa limekithiri. Fomu hiyo ilihitaji maelezo kadha,yakiwemo anwani ya afisi na ndugu wa karibu. Hatimaye, iwapo mtu angepatikana kuwa na virusi, wawasiliani wake wangefuatiliwa. Kulikuwa na vituo vya COVID-19 katika kila eneo la serikali ya mitaa na wafanyakazi wa afya waliokuwa na vifaa vya simu tayari kuwasaidia wale ambao hawakuwa na ufikiaji kwa vifaa vya kidijitali, japo wengi wa wafanyakazi hawa hawakuwa na ujuzi kwenye suala la kanuni ya usiri.

Data za watu waliokuwa na vipimo hasi au ambao walikuwa hawajawahi kuugua, pamoja na ndugu wa karibu, zilipakiwa kwenye hifadhidata ya mshiriki wa tatu, na kuzua swali la ni nani anayehifadhi data hizi, na kwa muda upi ukizingatia kutokuwepo kwa sheria za ulindaji data, kuwa bila jibu.

Kwa upande mwingine, Dayo, mhusika mwingine jijini Abuja, alikuwa na ushuhuda tofauti wakati NCDC ilipokuja kumpima na wenzake. Kulikuwa kumetokea mkurupuko ofisini kwake na kila mtu kupimwa. Dayo alielezea kuwa mchakato haukuwa wa kidijitali; "ulikuwa mchakato wa kawaida tu". Wawakilishi wa NCDC walikuja na fomu kadha zilizouliza maswali kadha na kwa Dayo, "mengi ya maswali hayo hayakuwa yenye umuhimu ila walikuja na mshauri kutafuta idhini yako. "Japo ilikuwa kana kwamba iliingilia faragha, niliona hoja". Kwa Dayo, haikuonekana kana kwamba maelezo yaliyokuwa yanakusanywa yangewekwa kwenye hifadhidata, angekuwa na wasiwasi kuhusu faragha yake na unyanyapaa ambao ungejitokeza na maelezo fulani. Dayo aliendelea  kusema kuwa uoga huu uliwafanya baadhi ya wenzake kujaza taarifa ghushi kwenye fomu za NCDC. Iwapo kutakuwa na utumiaji mbaya katika siku za usoni, kukosekana kwa sheria ya ulindaji data Nigeria kutawaweka Dayo na wengine kama yeye katika hali ya hatari.

Data za afya ya umma ni ya utambulisho wa kibinafsi na nyeti, inayotoa maelezo kuhusu mienendo ya mtu, tabia na afya. Sio tu kwa ushiriki wa serikali, bali pia washirika wa tatu wakiwemo waundaji programu na wanaojitolea wakati wa janga kufikia data za Wanigeria, kuna hitaji la wito wa uwajibikaji. Kuna hitaji la kugusia suala la haki ya faragha binafsi, haswa inayohusiana na masuala ya afya ya umma, na utumiaji wa haki za binadamu kwenye kuunda sera zenye uwezo wa kutokiuka haki za watu.

## Utafiti Maalum: Covid-19 Kiwango Cha Ufuatiliaji Mawasiliano: Mafunzo Kutoka Kwa Uzoefu Wa Nigeria

Imeandaliwa na Adeboye Adegoke, kwa ushirikiano wa Temitope Opeloyeru

Maisha yetu kwa sasa yanagubikwa kwa matumizi ya teknolojia, ambayo inafanya kazi eetu kuwa rahisi na za haraka, lakini teknolojia kamwe haibadilishi ubora wa kazi inayohitajika katika matumizi yake.

Kufuatia janga la COVID-19, ulimwengu ulitazama teknolojia kwa msaada kwani wadau mbali mbali walikuwa wakifanya kazi kuzuia wimbi la janga hilo, kulinda maisha na kufufua uchumi wa ulimwengu. Wakati virusi vilikuwa vinaenea haraka mnamo 2020 bila tiba bora ya kinga dhidi ya virusi au chanjo, ulimwengu ulilenga kudhibiti janga hilo kwa kuzuia. Kwa hivyo inaeleweka kuwa teknolojia ilizingatiwa kuwa muhimu kuwezesha mkakati wa kuzuia magonjwa. Google na Apple kampuni mbili za teknolojia zinazoongoza ulimwenguni, zilitangaza ushirikiano kwenye teknolojia ya kufuatilia maambukizi ya COVID-19 na zilichukua hatua za haraka kuhakikisha usalama wa faragha katika utoaji wao uliopendekezwa, ikithibitisha kuwa faragha na usalama wa mtumiaji ni muhimu kwenye muundo. Kuna ushahidi ulioandikwa wa ulindaji wa faragha katika kupitishwa kwa maombi ya kutafuta mawasiliano katika kusimamia COVID-19 na serikali za Ulaya. Jitihada hizo zinaweza kuwa zimechangia kupapasa kwa kiwango cha matukio yao, licha ya changamoto na kupitishwa kidogo, na wasiwasi wa faragha na usalama.

Nchini Nigeria, kama nchi nyingi za Kiafrika, serikali ilitangaza kufungwa, ilipendekeza utumiaji wa data ya rununu kwa uchunguzi wa COVID-19, ilianzisha sheria mpya, na zaidi. Hasa, kulikuwa na habari za maendeleo ya utaftaji wa mawasiliano ya kidijitali  wa Serikali na wasio wa serikali (State and non-state actors). Hizi ni hatua zilizo na athari wazi kwa haki za kidijitali, haswa haki ya faragha. Ili kuelewa ni kwa kiwango gani hatua za kufuatilia mawasiliano zilizokusanywa na serikali ya Nigeria, nilifanya utafiti ili kupata taarifa zinaohitajika. Nakala hii imejikita katika hadithi kutoka kwa watoa habari muhimu ambao ni wataalamu wa afya au waokoaji wa COVID-19 huko Abuja, Nigeria.

Dk Olajumoke Precious anafanya kazi kwa Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa cha Nigeria (NCDC) huko Abuja. Hajawahi kupima kuwa na virusi lakini

anaingiliana na wagonjwa. Maelezo yake ya hatua ya kutafuta mawasiliano iliyotumiwa na NCDC ni mwongozo. Anatambua kuwa mawasiliano ni kwa ajili ya ufuatiliaji, ambayo yanajumuisha kitambulisho, kuorodhesha, na kufuatilia watu fulani ambao wanaweza kuwa na mawasiliano au walikuwa karibu na mtu aliyeambukizwa. Kutokana na maelezo yake:

"Tunafanya hivyo kwa kuhoji shughuli za kesi ya maambukuzi, au shughuli na majukumu ya watu wanaozunguka kesi ya maambukizi, tangu kuanza kwa dalili. Tunachunguza pia maeneo yaliyotembelewa ndani ya siku 2-14 kabla ya kuanza kwa dalili. Tunatoa maelezo ya mawasiliano kama vile mtu huyo anaishi, watu wanaomzunguka, familia ya yule anayebeba maambukizi na wakati ambapo mtu amekufa, tunatembelea vituo vya afya ambapo marehemu alilazwa kabla ya kufariki ".

Kutoka kwa mtazamo wa manusura, Joseph Nikoro, mfanyabiashara wa mtandao na mkulima, alitoa nambari za simu za watu ambao alikumbuka aliwasiliana nao, kwa maafisa wa afya, na wakamwambia awapigie simu kuuliza ikiwa wamewasiliana na mtu mwingine yeyote. Ushahidi uliopo unaonyesha wazi kuwa teknolojia haikupata nguvu katika hatua hizi zote licha ya kuzunguka kwa ufanisi wa hatua za kutafuta mawasiliano ya kudhibiti, pamoja na njia za kutafuta mawasiliano ya kidijitali, na ushahidi kwamba programu hizo zilianzishwa nchini Nigeria.

Kuangalia mazingira ya haki za kidijitali nchini Nigeria, inatia wasiwasi kuona matumizi ya teknolojia kama hiyo ya ufuatiliaji wa kidijitali wakati wa maandamano kama maandamano ya Oktoba 2020 #EndSARS Wakati serikali ya Nigeria ikijitahidi kuonyesha ufanisi wa matumizi ya teknolojia kupambana na uhalifu, ugaidi, au kuzuia wimbi la janga linalowakilisha tishio kwa wanadamu - ambazo ni sababu ambazo kawaida huahidiwa kununua teknolojia hizi - haijawahi kufeli kutumia teknolojia hizi katika kulenga watetezi wa haki za binadamu, wakosoaji na waandamanaji. Kushindwa kwa serikali ya Nigeria kutafuta majambazi na magaidi, ambao wako katika kitovu cha changamoto za usalama wa nchi, bado ni kitendawili licha ya uwekezaji mkubwa katika teknolojia za ufuatiliaji. Jumla ya naira bilioni 9 (Dola za Marekani milioni 22.8) ilikadiriwa mwaka 2020 kugharamia shughuli na vifaa vinavyohusiana na ufuatiliaji.

Hatua ambayo wakosoaji wa serikali na waandamanaji wanafuatiliwa na kukamatwa kwa kidijitali hutoa dalili wazi ya hatari ya kuipatia serikali ambayo

ina historia ya kuzuia sauti zinazopinga nguvu ya kuingiliwa zaidi ili kufikia malengo yasiyo mema. Teknolojia hizi hazijatimiza madhumuni halisi zaidi ya kuwa zana za kutisha na unyanyasaji wa wale ambao wana maoni yanayopingana. Eromosele Adene bado anakabiliwa na kesi baada ya kufuatiliwa, kukamatwa, na kushtakiwa kwa kuhusika kwake katika maandamano ya #EndSARS. Salihu Tanko Yakasai alifuatiliwa, kukamatwa, na kufutwa kazi kwa kukosoa ushughulikiaji wa Rais wa maswala ya usalama nchini katika safu ya tweets, ambapo alimuomba Rais ajiuzulu.

Teknolojia si uchawi na ina uwezekano mkubwa wa kutumiwa kama zana ya kutisha na serikali ambazo zina ajenda za kukomesha wakosoaji. Ni chombo kinachofanya matumizi bora zaidi katika kutumikia malengo ya watendaji wenye bidii na wenye uwezo kwa hivyo muundo wa utawala ambao umegubikwa na uzembe na mielekeo mingine ya kupinga demokrasia hautatumia zana za ufuatiliaji kwa matumizi ya maendeleo. Badala yake, serikali hizo zitapata zana za teknolojia muhimu katika kufunga nafasi ya raia na kuzima sauti za upinzani. Hii ndio sababu ni muhimu kwa teknolojia na mazingira ya jamii kusisitiza juu ya mfumo mzuri wa sheria, uwajibikaji wa kimahakama, na uwazi wa lazima katika matumizi ya teknolojia ya ufuatiliaji.

# LONDA

**NIGERIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

PARADIGM
INITIATIVE

**Paradigm Initiative**

374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria

Email: media@paradigmhq.org

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ